



TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Tarehe: 19 Mei 2023

1. Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA) inategemea kuondosha vifaa chakavu kwa njia ya mnada wa hadhara.
2. Vifaa hivyo ni kama vifuatavyo:-
 - a) Makangavuke (Generators)
 - b) Vifaa vya Tehama
 - c) Vifaa vya ofisini na
 - d) Samani
3. Minada itafanyika katika maeneo ya Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA), Chang'ombe Central Store, Saza road, Dar Es Salaam, Uwanja wa Ndege Songwe, Uwanja wa Ndege Tabora, Uwanja wa Ndege Tanga, Uwanja wa Ndege Pemba na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Amani Abeid Karume (AAKIA).
4. Tarehe za mnada kwa kila eneo ni kama ifuatavyo:

| Na. | Mahali | Tarehe ya mnada |
|-----|---|-----------------|
| 1. | Chang'ombe Central Store, Saza road, Dar Es Salaam | 2 Juni 2023 |
| 2. | Uwanja wa Ndege Songwe | 17 Juni 2023 |
| 3. | Uwanja wa Ndege Tabora | 17 Juni 2023 |
| 4. | Uwanja wa Ndege Tanga | 17 Juni 2023 |
| 5. | Uwanja wa Ndege Pemba | 17 Juni 2023 |
| 6. | Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Amani Abeid Karume (AAKIA) | 17 Juni 2023 |

MASHARTI YA MNADA

- a) Chombo/Kifaa kitauzwa kama kilivyo na mahali kilipo.
- b) Atakayetaja bei ya juu kabla ya nyundo kugongwa ndiye atakayeuziwa kifaa.
- c) Aliyetaja bei ya juu siyo lazima auziwe kama bei hiyo haijafikia bei elekezi.
- d) Kwa makangavuke, Mnunuzi atatakiwa kulipa papohapo asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya kangavuke alilonunua. Asilimia sabini na tano (75%) iliyobakia atatakiwa kulipa ndani ya siku kumi na nne (14). Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hili atakosa haki zote za ununuzi wa kangavuke husika.
- e) Kwa vifaa na samani, Mnunuzi atatakiwa kulipa papohapo asilimia miamoja (100%) ya thamani ya chombo/kifaa alichonunua. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hili atakosa haki zote za ununuzi wa chombo/kifaa husika.
- f) Mnunuzi ataruhusiwa kuchukua vifaa vyake kutoka maeneo ya Mamlaka ya Usafiri wa Anga yalitotajwa hapo juu baada ya kukamilisha malipo yote.

LIMETOLEWA NA:

**MKURUGENZI MKUU,
MAMLAKA YA USAFIRI WA ANGA TANZANIA,
JENGO LA MAMLAKA YA USAFIRI WA ANGA,
MAKUTANO YA BARABARA YA NYERERE NA KITUNDA,
S.L.P 2819,
DAR ES SALAAM.**